

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI

23 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI TAREHE 23 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

416. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kujenga Vituo vya Afya Kata za Kandawale, Kibata, Namanyuni, Mingumbi na Kinjumbi - Kilwa.

**417. MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU
(KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Kibamba.

**418. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI
(MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa madarasa Shule za Msingi Ikunguipina, Izimbili, Mwina, Itibula, Ndembezi, Chapela na Bulangamilwa - Manonga.

**419. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI
(MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Madaraja ya Chiwachiwa, Mbasu, Isago na Mfuji - Mlimba.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

420. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali italipa Kifuta Machozi kwa Wahanga wa Wanyama waharibifu – Bunda Mjini.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

421. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaanzisha mafunzo ya ufugaji wa kisasa kwa Wafugaji ngazi ya Kata ili kuwa na ufugaji wenye tija.

422. MHESHIMIWA FURAHA NTENGO MATONDO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itavipatia mafunzo vikundi vya *Beach Management Unit* ili kukabiliana na uvuvi haramu.

WIZARA YA UJENZI:

423. MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (MBARALI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Rujewa - Madibira hadi Mafinga yenye urefu wa Km 151.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

424. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALLOS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kuna mpango gani wa kushughulikia kwa haraka mashauri ya ndoa kuepuka utelekezaji wa familia na vitendo vya ukatili na unyanyasaji.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

425. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali imefikia wapi katika maandalizi ya AFCON 2027 kwenye ujenzi wa Viwanja na Hoteli nchini.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
23 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

